**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**Bodi ya Usajili wa Wathamini**

**Chuo Kikuu cha Dodoma, shule ya CIVE**
**Jengo la Utawala, Ghorofa ya 1,**
**S. L. P. 325, Dodoma, Tanzania**
**Simu Na: +255 733542654,**
**Barua pepe: registrar@vrb.go.tz**

Integrity and Fairness

# MAHAFALI YA TATU YA WATHAMINI WALIOHITIMU MAFUNZO YA USAJILI KAMILI, SIKU YA IJUMAA TAREHE 31 MEI, 2024

Kwa mujibu wa mamlaka yaliyotolewa na Kanuni Na. 44(1) ya Kanuni za Mafunzo na Mitihani kwa Wathamini za mwaka 2020, Msajili anapenda kuwatangazia Wathamini na umma kwa ujumla kuwa Bodi itagawa vyeti kwa Wathamini wahitimu wa mafunzo ya usajili kamili wa wathamini katika Mahafali ya Tatu ya Bodi yatakayofanyika siku ya tarehe 31/05/2024 jijini Dodoma.

Sherehe za Mahafali zimepangwa kuanza rasmi saa tatu kamili asubuhi na zitahudhuriwa na viongozi mbalimbali, wathamini na wageni waalikwa. Gharama za kushiriki katika Mahafali haya ni Tshs.200,000/= kwa kila mhitimu. Hivyo, wahitimu wote wanatakiwa kuthibitisha ushiriki wao kwa kulipa ada hiyo kabla ya tarehe 20/05/2024.

Ratiba kamili na ukumbi utakaofanyikia mahafali hayo itatangwaza hapo mbeleni. Kupata kumbukumbu namba ya malipo au maelezo zaidi, tafadhali wasiliana nasi kupitia simu 0733542654, 0654103361 au barua pepe; registrar@vrb.go.tz

**MSAJILI WA BODI**

7 Mei 2024